*Kioo cha Lugha, Juz. 20 (2), 257-268*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v20i2.7

# Tathmini ya Matumizi na Kukubalika kwa Istilahi za Simu kwa Wazungumzaji wa Kiswahili Nchini Tanzania

*Majura Nyangaywa*[1] na *Pendo S. Malangwa*[2]

**Ikisiri**

Makala hii inaangazia hali ya matumizi na kukubalika kwa istilahi za Kiswahili za simu za mkononi miongoni mwa wazungumzaji wa Kiswahili nchini Tanzania. Data zilikusanywa kwa mbinu ya usomaji matini, hojaji na usaili kutoka kwa watoataarifa katika kata za Kimara na Ubungo, Dar es Salaam. Nadharia ya Ulinganifu wa Kiathari ilitumika katika makala hii. Matokeo yanaonesha kuwa baadhi ya wazungumzaji wanakubali kutumia istilahi za Kiswahili za simu na wengine hawakubali. Aidha, makala inabainisha sababu mbalimbali zilizotolewa na kila upande. Makala inapendekeza kuwapo kwa ushirikishwaji wa wazungumzaji wa Kiswahili, wataalamu wa teknolojia ya mawasiliano na wataalamu wa istilahi wakati wa mchakato wa uundaji wa istilahi za Kiswahili za simu za mkononi.

## 1.0 Utangulizi

Simu za mkononi zina programu zenye istilahi za lugha chanzi, kama vile Kifini (*Nokia*), Kichina (*Tecno*) na Kiingereza (*Apple*) zilizobuniwa awali na watengenezaji (Okyere na wenzie, 2016). Kamau (2007) anaeleza kuwa usambazaji na utumiaji wa teknolojia ya mawasiliano, zikiwamo kompyuta na simu, hutegemea lugha. Nchi nyingi za Kiafrika hupokea teknolojia hii kwa lugha za kigeni. Kamau anafafanua zaidi kuwa watumiaji wengi waliolengwa kutumia teknolojia hii katika Bara la Afrika, hawawezi kuzitumia istilahi hizi kwa kuwa baadhi yao hawazielewi zikiwa katika lugha chanzi. Katika hali kama hii, kunatokea haja ya kuhawilisha istilahi za teknolojia ya mawasiliano kwa kuzijanibisha katika lugha za Kiafrika ili ziweze kutumiwa na walengwa wa vifaa vya mawasiliano vinavyohitajika. Akishadidia jambo hili, Sanday (2014) anaeleza kuwa ujanibishaji wa lugha za kigeni katika lugha za Kiafrika kupitia teknolojia ya mawasiliano unawezesha kuondoa vikwazo vya lugha kwa wasioelewa vyema lugha za kigeni.

[1] Mhadhiri Msaidizi, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Kigamboni, Tanzania. Baruapepe: nyangaywa@yahoo.co.uk
[2] Profesa Mshiriki, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: malangwa2011@rocketmail.com au pmalangwa@udsm.ac.tz

Kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali, shughuli ya kuunda istilahi za uga wowote hulenga kuunda istilahi zinazozingatia sifa mahususi. Kwa mfano, Felber (1980) anaeleza sifa za istilahi sadifu kuwa ni: usahihi, ufupi, urahisi wa kutamkika na kuandikika, urahisi wa kunyambuka, uzingativu wa sarufi ya lugha lengwa, uwakilishi wa dhana moja tu na udhana. Aidha, Tumbo-Masabo na Mwansoko (2008) wanapendekeza misingi mahususi inayopaswa kuzingatiwa katika uundaji wa istilahi. Misingi hiyo ni pamoja na: istilahi kuakisi sifa bainifu za dhana zinazowakilishwa, istilahi kuweza kunyambulika ili kuwezesha kuundwa kwa istilahi zingine za kikoa hichohicho, istilahi zenye vivuli vya maana zinazoingiliana kuwa na ulinganifu wa mtiririko, istilahi kuwa na utoshelevu na ufupi ili kuziwezesha kueleweka kirahisi, istilahi mahuluti na finyazo kuepukwa na kila istilahi kuwakilishwa na dhana moja tu. Kwa misingi hiyo, inatarajiwa kwamba istilahi za teknolojia ya mawasiliano zinapoundwa zikidhi haja hizo.

Licha ya istilahi za Kiswahili za simu kuendelea kuundwa na kutumiwa na baadhi ya wazungumzaji wa Kiswahili, bado zinahitaji kufanyiwa uchunguzi ili kubainisha hali ya matumizi na kukubalika kwake miongoni mwa watumiaji wa simu. Tafiti zilizofanywa na wataalamu (taz. Kihore 2000; Malangwa, 2010; Ibrahimu, 2017; Malangwa 2019) zinaonesha kuwa baadhi ya istilahi zinakubaliwa na zingine hazikubaliwi. Kwa mfano, Kihore (2000) ametilia shaka ukubalifu wa istilahi za Kiswahili za kompyuta. Anapendekeza kwamba kuna haja ya kutazama suala la istilahi za Kiswahili za kompyuta kwani kuna maneno kadhaa yaliyojitokeza ambayo hayakutafutiwa visawe vyake kwa Kiswahili. Kihore anaongeza kuwa hata pale vilipotolewa visawe, ni dhahiri kuna haja ya kuvitazama upya kwa mtazamo mpana zaidi wa matumizi miongoni mwa wazungumzaji wa Kiswahili.

Naye Malangwa (2010) anafafanua kuwa mkanganyiko wa istilahi za kiufundi zinazoundwa au kutafsiriwa, unasababishwa na ushirikiano hafifu miongoni mwa wataalamu wa lugha. Wataalamu hawa hujumuisha walimu wafundishao lugha, wanateminografia na wanaleksikografia. Malangwa anaongeza kuwa sababu nyingine ya mkanganyiko wa istilahi za kiufundi ni mbinu tenge zinazotumiwa katika tafsiri ambapo hutokeza istilahi moja katika lugha chanzi kuwa na visawe zaidi ya kimoja katika lugha lengwa. Akishadidia jambo hili, Kinyanjui (2014) anatoa mifano ya istilahi zilizoundiwa kisawe zaidi ya kimoja ikiwamo *monitor* yenye visawe: *monita, kiwaa, kiwambo na mulishi*. Istilahi zingine ni *setting* yenye visawe: *kipimo, mpangilio na mpangizo*. Kadhalika, *recyclebin* ina visawe *kisaduru, kijalala na urejelezaji*.

Kuwapo kwa visawe vingi vinavyowakilisha istilahi moja katika lugha chanzi huchukuliwa kuwa mkanganyiko wa istilahi unaojitokeza kwa wazungumzaji wa Kiswahili. Katika hali kama hiyo, wazungumzaji wa lugha lengwa wanashindwa kujua ni istilahi ipi itumiwe katika mazungumzo yao ya kila siku wanaporejelea dhana mahususi. Kwa kuzingatia msingi huo, makala hii inaangazia tathmini ya matumizi na kukubalika kwa istilahi za Kiswahili za simu

kwa wazungumzaji wa Kiswahili watumiao simu za mkononi nchini Tanzania. Vigezo vya tathmini vimejengwa katika kuangalia: je, istilahi zilizoundwa zimezingatia sifa na misingi ya uundaji wa istilahi zilizobainishwa na wataalamu? Je, hali ya upokelewaji wa istilahi za simu kwa wazungumzaji ikoje? Je, watumiaji wa simu wanatoa sababu gani za kukubali kutumia au kutotumia istilahi za Kiswahili? Je, masuala ya kinadharia yamezingatiwa katika istilahi za Kiswahili za simu?

## 2.0 Kiunzi cha Nadharia


Makala hii imetumia Nadharia ya Ulinganifu wa Kiathari. Hii ni nadharia ya tafsiri ya kimawasiliano iliyoasisiwa na Nida mwaka 1964 na kusasishwa na Nida na Taber (1969). Kwa mujibu wa Nadharia ya Ulinganifu wa Kiathari, mfasiri hukusudia kudumisha athari ileile na kuhakikisha hadhira ya lugha lengwa ina mwitikio sawa na hadhira ya lugha chanzi. Kwa mantiki hiyo, mwitikio wa hadhira ya lugha lengwa ni muhimu uwe kama wa hadhira ya lugha chanzi. Mfasiri huchukua mawazo ya lugha chanzi na kuyahamisha katika lugha lengwa kwa muundo na mtindo unaoleta athari na mwitikio sawa. Mfasiri (ambaye katika muktadha wa makala hii ni muundaji wa istilahi za simu) atafute visawe (istilahi za Kiswahili za simu) vya karibu zaidi na ujumbe wa lugha chanzi ili kuwezesha hadhira lengwa (ambayo katika makala hii ni wazungumzaji wa Kiswahili wanaotumia simu za mikononi) kufahamu maana za visawe (yaani, istilahi za simu) za programu za simu za mkononi. Nadharia hii ilitumika kupambanua hali ya matumizi na kukubalika kwa istilahi za simu miongoni mwa wazungumzaji wa Kiswahili nchini Tanzania.

## 3.0 Mbinu za Utafiti

Mbinu za utafiti huu zilijumuisha usampulishaji, ukusanyaji na uchambuzi wa data, pamoja na uwasilishaji na matokeo. Katika sehemu hii tutaeleza kwa kifupi mbinu hizi na jinsi tulivyozitumia. Mbinu ya usampulishaji sahili ilitumika kupata watumiaji sitini na wanane wa simu wanaozungumza Kiswahili. Eneo lililotumika kupata data ni kata za Kimara na Ubungo, manispaa ya Ubungo, jijini Dar es Salaam. Mchakato wa kuwapata watumiaji wa simu ulizingatia utayari, utumizi wa simu za mkononi na ujuzi wa kusoma na kuandika Kiswahili kwa watoataarifa. Data zilikusanywa kwa mbinu ya usomaji wa matini, hojaji na usaili. Mbinu ya usomaji matini ilitumika kukusanya istilahi za programu za simu.Aina za simu zilizotumika ni *Nokia*, *Itel* na *Tecno*. Kupitia mbinu hii tulipata istilahi za simu kwa lugha za Kiswahili na Kiingereza kisha kuzipanga kwa mpangilio wa alfabeti. Aidha, mbinu ya hojaji ilitumika kukusanya data kwa watumiaji wa simu sitini na wanane waliozijaza na kuzirejesha. Hojaji hizi zilihusu matumizi ya istilahi, upokelewaji na kukubali kutumia au kutotumia istilahi za Kiswahili za programu za simu. Usaili ulihusu watumiaji wa simu kubainisha sababu za kutumia au kutotumia istilahi za Kiswahili za simu katika simu zao. Data zilichambuliwa na kuwasilishwa kwa mikabala ya kitaamuli na kitakwimu.

## 4.0 Hali ya Matumizi na Kukubalika kwa Istilahi za Simu kwa Wazungumzaji wa Kiswahili

Matumizi ya istilahi za simu kwa wazungumzaji wa Kiswahili ni jambo lililoshughulikiwa kimuktadha katika makala hii kurejelea wanaokubali au wasiokubali kutumia istilahi za Kiswahili za simu. Ufafanuzi umetolewa kitakwimu ili kuonesha hali ilivyo kwa wazungumzaji wa Kiswahili wanaotumia istilahi za simu za Kiswahili. Ili kufahamu matumizi ya istilahi hizo, watoataarifa sitini na wanane waliulizwa swali hili: "simu yako ya mkononi unaitumia ikiwa katika lugha gani?" Lengo la swali hili lilikuwa kufahamu ni lugha ipi hasa inatumiwa na wengi kati ya Kiswahili, Kiingereza au lugha nyinginezo katika programu za simu. Matokeo yanaonesha kuwa mtoataarifa mmoja anatumia lugha ya Kifaransa ingawa anazungumza Kiswahili pia. Watoataarifa watano walisema wanatumia lugha ya Kiswahili. Watoataarifa sitini na wawili walisema wanatumia lugha ya Kiingereza. Kielelezo Na. 1 kinaonesha hali ya matumizi na kukubalika kwa istilahi za simu kwa wazungumzaji:




**Kielelezo Na. 1:** *Matumizi na Kukubalika kwa Istilahi za Simu kwa Wazungumzaji*

Kielelezo Na. 1 kinaonesha hali ya matumizi ya istilahi za simu miongoni mwa wazungumzaji wa Kiswahili. Mtoataarifa mmoja sawa na asilimia 1.4 anatumia simu katika lugha ya Kifaransa ingawa anazungumza pia Kiswahili. Vilevile, watoataarifa watano sawa na asilimia 7.35 wanatumia Kiswahili katika programu za simu. Aidha, watoataarifa sitini na wawili sawa na asilimia 91.17 wanatumia Kiingereza katika programu za simu zao. Matokeo haya yanatoa taswira ya hali ya matumizi ya istilahi za Kiswahili za simu za mkononi. Ilitarajiwa kwamba istilahi za Kiswahili zipokelewe na kutumiwa na wengi miongoni mwa wazungumzaji wa Kiswahili. Matokeo katika data ni kinyume chake. Hali hii ilichochea waandishi wa makala hii kuchunguza zaidi kuhusu sababu za mtawanyiko huo wa kimatumizi. Sehemu inayofuata inadhihirisha sababu za watoataarifa kutumia au kutokutumia istilahi za Kiswahili katika simu zao.

### 4.1 Sababu za Kutumia Kiswahili katika Simu

Kundi la kwanza lilikubali kuwa linatumia lugha ya Kiswahili katika programu za simu. Maelezo zaidi kuhusu sababu za kundi hili yametolewa katika sehemu zinazofuata.

#### 4.1.1 Uelewekaji wa Kiswahili kwa Watumiaji

Watoataarifa watano kati ya sitini na wanane sawa na asilimia 7.35 walidai kuwa wanatumia lugha ya Kiswahili katika programu za simu kwa kuwa wanaielewa vyema. Watoataarifa hao waliongeza kuwa lugha ya Kiswahili imezoeleka kwa walio wengi ikilinganishwa na lugha nyinginezo, kikiwamo Kiingereza. Hata katika kutoa sababu hii, watoataarifa walilinganisha uelewa wao wa haraka kati ya Kiswahili na Kiingereza. Mmoja wa watoataarifa alikuwa na haya ya kusema:

> …Kiswahili ni lugha ambayo inanitambulisha utaifa wangu wa Tanzania, kwa sababu ndio lugha niliyoitumia sana sehemu ya maisha yangu toka ninaanza shule ya msingi hadi kumaliza. Hivyo, nimezoea kuitumia lugha hii na watu wengi ninaokutana nao tunatumia lugha hiyo...

Mtoataarifa huyu anaonesha kwamba anaitumia lugha ya Kiswahili mara kwa mara. Kwa hiyo, ni rahisi kwake kuwasiliana kwa Kiswahili na watu wengine kuliko lugha nyingine. Maelezo ya watoataarifa yana mashiko yakilinganishwa na matumizi ya Kiswahili nchini Tanzania. Uamuzi wa serikali kutumia Kiswahili kama lugha ya taifa na kutambua umuhimu wa utamaduni na lugha, umewafanya watumiaji kuwa na uhuru wa kujieleza na kuwasiliana kwa urahisi. Mawazo kama haya yanashadidiwa na Maganga (2008) kuwa baada ya kupata uhuru wa Tanzania Bara, Kiswahili kilipandishwa hadhi na kuteuliwa kuwa lugha ya taifa. Kutokana na hatua hiyo, Kiswahili kikaanza kutumika katika mijadala bungeni na hatimaye kuwa lugha ya kufundishia katika shule za msingi. Hatua ya kupandisha hadhi lugha ya Kiswahili na kuifanya lugha ya taifa kumeifanya itumiwe na watu wengi na hivyo kueleweka kwao kama watoataarifa walivyobainisha. Kwa hiyo, hii ni sababu iliyowafanya waamue kutumia istilahi za Kiswahili za programu za simu za mkononi katika simu zao.

#### 4.1.2 Ugumu wa Lugha ya Kiingereza

Watoataarifa watano kati ya sitini na wanane sawa na asilimia 7.35 walisema kwamba wanatumia lugha ya Kiswahili kwa sababu Kiingereza ni lugha yenye msamiati mgumu zaidi ikilinganishwa na Kiswahili. Mathalani, mmoja wa watoataarifa alisema:

> …Lugha ya Kiingereza ni ngumu kwangu, ninaelewa maneno machache sana kuliko lugha ya Kiswahili. Pia, watu walio wengi wanafahamu lugha ya Kiswahili zaidi kuliko Kiingereza...

Maelezo ya mtoataarifa huyo yanaonesha namna lugha ya Kiingereza ilivyo ngumu kimatumizi ikilinganishwa na ya Kiswahili. Ugumu huo unatokana na hoja kwamba maneno ya lugha ya Kiingereza hutamkwa tofauti na yanavyoandikwa (Crystal, 2012). Kwa mfano, maneno kama vile *password* na *missed calls*, kimsingi yanavyoandikwa ni tofauti na yanavyotamkwa. Hii ni tofauti na maneno ya lugha ya Kiswahili ambayo jinsi maneno yanavyoandikwa ndivyo yanavyotamkwa, mathalani, maneno kama vile: simu, kitufe na ujumbe. Mifano hii inathibitisha kuwa hoja zilizotolewa na watoataarifa ni za msingi na zinajibainisha wazi katika programu za simu teule. Madai haya yanawiana na mawazo yaliyomo katika Nadharia ya Ulinganifu wa Kiathari kwamba mfasiri atafute visawe vya karibu zaidi na ujumbe wa lugha chanzi ili kuwezesha hadhira lengwa kupata athari ileile kama ilivyo kwa hadhira ya lugha chanzi. Kwa mantiki hiyo, watumiaji wa Kiswahili wanaotumia simu za mkononi wanapata athari ileile ya kimaana katika lugha lengwa kama ilivyo katika lugha chanzi kama inavyosisitizwa na nadharia hii.

### 4.2 Sababu za Kutumia Lugha ya Kiingereza katika Simu

Kundi la pili lilieleza kuwa linatumia Kiingereza katika simu. Kundi hili lilikuwa na jumla ya watoataarifa 62 kati ya 68 walioshiriki katika utafiti huu. Sababu za uamuzi wa kutumia lugha ya Kiingereza katika simu unahalalisha pia kutumia istilahi za Kiingereza za simu za mkononi. Sehemu inayofuata inafafanua sababu zilizotolewa na kundi hili.

#### 4.2.1 Maneno ya Kiswahili kwenye Simu ni Tofauti na Yaliyozoeleka

Watoataarifa thelathini na wawili kati ya 68 sawa na asilimia 47.05 walidai kuwa maneno ya Kiswahili yaliyoko katika programu za simu za mkononi ni tofauti na Kiswahili cha kawaida. Waliendelea kufafanua kwamba istilahi za simu za mkononi za Kiswahili ni ngumu kueleweka kwao. Akisisitiza suala la maneno ya Kiswahili yaliyoko kwenye simu za mkononi kuwa ni magumu, mmoja wa watoataarifa alisema:

> …Maneno ya Kiswahili yaliyoko kwenye simu ya mkononi ni magumu kwelikweli. Kiswahili kinachoongelewa katika jamii ni tofauti na na maneno yaliyopo kwenye programu za simu. Kiswahili cha simu ni fasaha na huwashinda watu wengi…

Watoataarifa waliongeza kuwa maneno yanayotumiwa kwenye programu za simu ni kana kwamba yanatoka kiwandani au maabarani, ambako hakuna jamii ya wasemaji lugha. Jedwali lifuatalo linaonesha baadhi ya istilahi za Kiswahili za programu za simu zilizobainishwa na watoataarifa kuwa ni ngumu kueleweka:

**Jedwali Na.1: Baadhi ya Istilahi Ngumu Zilizobainishwa na Watoataarifa**

| **Na.** | **Istilahi za Kiswahili** | **Istilahi za Kiingereza** |
|---|---|---|
| 1. | sasisha | *updates* |
| 2. | gotoka | *deny* |
| 3. | nywila | *password* |
| 4. | pasiwaya | *wireless* |
| 5. | msimbo | *code* |
| 6. | kivinjari | *browser* |
| 7. | arifa | *notification* |
| 8. | mswada jaribu | *draft* |
| 9. | ufungaji baobonye kiotomatiki | *auto keypad lock* |
| 10. | huduma ya kuzuia simu | *call barring service* |
| 11. | ruhusu kipaumbele pekee | *priority only allows* |

**Chanzo:** Data za Uwandani (Julai 2021)

Jedwali Na.1 linadhihirisha mifano ya istilahi zilizobainishwa na watoataarifa kuwa ni ngumu. Watoataarifa wanaziona istilahi hizi kuwa ni ngeni na hawajawahi kuzisikia. Hivyo, wanaziona kwenye simu na wanashindwa kuelewa kuwa zinafumbata dhana gani kimatumizi. Watoataarifa walisema ni bora watumie istilahi za Kiingereza hata kama ni kwa kutohoa na kutafsiri wajuavyo kuliko kutumia istilahi za Kiswahili ambazo hawazielewi. Kwa sababu hiyo, wazungumzaji wanapata ugumu wanapoteua Kiswahili kutumiwa katika programu za simu. Massamba (1997) anaeleza kwamba mojawapo ya sababu za kutokubaliwa kwa istilahi za Kiswahili ni kuwa watumiaji wanaona wanaistilahi wameunda maneno mapya ambayo ni magumu kwao. Massamba anatolea mfano wa watumiaji wanaosikika wakisema, 'hawa wataalamu wa Kiswahili wanakifanya Kiswahili kuwa kigumu mno'. Massamba anaendelea kueleza kwamba hapa watumiaji wanamaanisha kuwa wanataka istilahi kuwekwa katika lugha ya kawaida waliyoizoea.

Matokeo ya watoataarifa yanaibua mjadala unaohitaji tutafakari kuhusu suala la uundaji wa istilahi za simu. Tukichunguza data zilizotolewa kwenye Jedwali Na.1, tunabaini kuwapo kwa changamoto mbalimbali kama ifuatavyo. Kwanza, sifa na misingi iliyobainishwa na wataalamu haina budi kuzingatiwa. Baadhi ya istilahi zilizolalamikiwa na wazungumzaji kuwa ni ngumu zimeundwa zikiwa zimekiuka baadhi ya sifa na misingi ya uundaji wa istilahi. Kwa mfano, sifa na msingi wa istilahi kuwakilishwa na dhana moja. Inatarajiwa kuwa istilahi zinazoundwa katika uga wowote ziwakilishe dhana moja. Hali hii ni tofauti kwa baadhi ya istilahi zilizotajwa katika Jedwali Na. 1. Mathalani, istilahi *nywila* katika simu ya Tecno, itokanayo na istilahi *password* katika Kiingereza ina kisawe cha *nenosiri* katika simu ya Itel. Istilahi *chelezo* katika simu ya Itel itokanayo na

istilahi *data* katika Kiingereza ina kisawe cha *data* katika simu ya Tecno. Istilahi *mswada jaribu* katika simu ya Itel itokanayo na istilahi *draft* katika Kiingereza ina kisawe cha *rasimu* katika simu ya Nokia. Kwa ujumla, hii ni changamoto na inaibua mkanganyiko kwa watumiaji wa simu inapotokea istilahi katika lugha chanzi kuwa na visawe zaidi ya kimoja katika lugha lengwa. Suala la dhana iwakilishwayo katika kisawe zaidi ya kimoja linaleta utata na mkanganyiko kwa wazungumzaji wa Kiswahili wanaotumia simu.

Madai ya watoataarifa kuwa baadhi ya istilahi za Kiswahili ni ngumu na hawazielewi si ya kupuuzwa. Madai yenye maudhui kama haya yamewahi kutolewa pia na Kinyanjui (2014) akifafanua kwamba istilahi zinapowekwa wazi kulingana na dhana, utata na mkanganyiko unaweza kuepukwa. Anaendelea kufafanua kuwa istilahi zisipoeleweka zitafanya mawasiliano yakatike na yakwame kati ya watumiaji. Kwa hiyo, kuna kila sababu ya kufanya usanifishaji na ulinganishaji wa istilahi zilizoundwa kama ambavyo baadhi ya wataalamu wamewahi kushauri (taz. Mdee, 1999; Massamba, 2007; Kahigi, 2007; Kevogo, 2016).

Pili, msingi uliokiukwa katika data hizo ni baadhi ya istilahi kutokuwa fupi. Baadhi ya istilahi zilizopo katika data hizo ni ndefu kiasi kwamba zinakinzana na misingi iliyobainishwa. Vilevile, urefu wa istilahi hizo unazifanya zikose sifa ya kunyambulika ili kuunda istilahi nyingine za kikoa hichohicho kama ilivyobainishwa na watalaamu (taz. Felber, 1980; Kahigi, 2007; Tumbo-Masabo na Mwansoko, 2008). Kwa mfano, istilahi *mpangilio wa kilinda vitufe* yenye kisawe *keyguard setting* ina maneno manne katika lugha lengwa ilhali katika lugha chanzi ina maneno mawili tu. Pia, istilahi *mwanga wa nyuma wa baobonye* yenye kisawe *keypad backlight* ina maneno matano katika lugha lengwa ilhali katika lugha chanzi ina maneno mawili tu. Istilahi hizi ni ndefu, hivyo, haziwezi kunyambulika ili kuruhusu uundwaji wa istilahi nyingine za kikoa hichohicho kama msingi wa uundaji wa istilahi unavyoelekeza. Kilichotarajiwa ni waundaji kuweka tafsiri kwa kuzingatia iktisadi ili kufanya istilahi ziwe fupi. Hivyo, istilahi za Kiswahili za simu zilizoundwa ili zitumike katika simu, baadhi zinaonekana hazikidhi mahitaji ya watumiaji wa simu wanaozungumza Kiswahili. Wazungumzaji wanaona ni maneno mageni kwao. Hali hii ya istilahi kuonekana ngumu kueleweka na kukiuka baadhi ya misingi ya uundaji wa istilahi inadokeza kwamba zina changamoto. Pia, baadhi hazikubaliwi na watumiaji wa lugha lengwa.

### 4.2.2 Uelewekaji wa Istilahi za Kiingereza kwenye Simu

Watoataarifa 38 kati ya 68 sawa na asilimia 55.88 walisema kuwa istilahi za Kiingereza zilizoko kwenye simu za mkononi zinaeleweka kwa urahisi zaidi kuliko istilahi za Kiswahili. Jambo hili lilichochea haja ya kutaka kujua zaidi kwa nini watoataarifa waelewe Kiingereza kuliko Kiswahili. Watoataarifa waliongeza kuwa hali hii inatokana na jinsi simu zao zilivyokuwa na muundo wa istilahi za

lugha ya Kiingereza tangu wamezinunua na kuwafanya wajizoeze kuzitumia kuliko istilahi za Kiswahili zilizoundwa baadaye. Kwa hiyo, wamekuwa wakitumia istilahi za Kiingereza za programu za simu mara kwa mara kuliko Kiswahili. Mmoja wa watoataarifa alisema:

> Kwa sababu lugha ya Kiingereza kwenye simu misamiati yake inaeleweka sana kuliko ile ya Kiswahili. Kiingereza ni lugha ambayo hainipi shida kuielewa maana maneno yaKiswahili kwenye simu kwangu bado ni tatizo...

Watoataarifa walieleza kuwa simu zilizo nyingi, zilizoanza kuingizwa nchini Tanzania na Afrika Mashariki, hazikuwa na lugha ya Kiswahili badala yake zilikuwa na Kiingereza kama lugha chanzi. Kwa sababu hiyo, baadhi ya watumiaji wa simu walizoea kutumia istilahi za Kiingereza za simu kuliko za Kiswahili. Suala hilo limewafanya kuzizoea istilahi za Kiingereza japokuwa ni kwa kukariri ili kufanikisha mawasiliano. Suala la kuzoea istilahi za Kiingereza zilizopo katika simu kwa kukariri limewahi kuelezwa pia na Kevogo (2016) akibainisha kuwa mazoea ya kukariri istilahi za Kiingereza za simu yamewafanya watumiaji wa simu waanze kujiundia istilahi zao watakavyo hata kama hazitambuliki katika mfumo rasmi.

### 4.2.3 Kutumia Lugha ya Kiswahili katika Programu za Simu ni Ushamba

Mtazamo hasi dhidi ya lugha ya Kiswahili walionao baadhi ya wazungumzaji ulijidhihirisha katika makala hii. Watoataarifa watatu kati ya sitini na wanane sawa na asilimia 4.41, walisema kuwa hawatumii istilahi za Kiswahili za simu kwa kuwa huo ni ushamba. Sababu hii inatia shaka kwa kuwa watumiaji wa simu ambao pia ni wazungumzaji wa Kiswahili wanajaribu kukana lugha yao. Mtoataarifa mmoja alisema:

> …Jamii ya Tanzania tumetawaliwa na ukoloni, hivyo tunajiona kuwa kutumia Kiswahili ni kujitweza. Kwa hiyo, kutumia Kiswahili katika simu za mkononi, utaonekana uko nyuma na wala si wa kisasa…

Kulingana na watoataarifa, lugha ya Kiingereza iliyoko kwenye simu inaonekana ni ya kisasa kuliko lugha nyingine. Suala la watu kukana lugha na tamaduni zao limewahi kusemwa na Qorro (2007) akieleza kuwa mtu kuikana lugha yake ni suala la kisaikolojia linalomfanya asijiamini na akose mahali pa kuanzia. Anaongeza kwamba, mtu anayekana mambo yake hajiamini kama amekamilika mpaka akamilishwe na ya wengine. Anasisitiza kwamba ili mtu akamilike anapaswa ajiamini na ajithamini ikiwa ni pamoja na kuthamini vya kwake, ikiwamo lugha yake.

Matokeo haya yanadokeza kuwa baadhi ya wazungumzaji wa Kiswahili wanaotumia simu bado hawaoni umuhimu wa kutumia Kiswahili katika simu zao. Mtazamo hasi walionao wazungumzaji wa Kiswahili dhidi ya matumizi ya Kiswahili umeenea miongoni mwa watu wa Afrika Mashariki. Kamau (2007)

anabainisha kuwa wazungumzaji wengi wa Kiswahili wana mtazamo hasi dhidi ya lugha hiyo. Hii ndiyo maana wanapendelea kutumia Kiingereza katika teknolojia ya mawasiliano na miktadha rasmi. Kamau anaendelea kufafanua kwamba jambo hili linadhihirika zaidi katika nchi za Uganda na Kenya. Hata hivyo, makala hii imeonesha pia kuwa nchini Tanzania baadhi ya wazungumzaji wana mtazamo hasi dhidi ya matumizi ya Kiswahili katika simu. Hali hii imejidhihirisha katika hoja kuwa kutumia istilahi za Kiswahili katika programu za simu ni ushamba kama ilivyobainishwa na watoataarifa. Matokeo haya yana maana kwamba zinahitajika juhudi za pamoja zitakazoshirikisha wadau wa Kiswahili, vyombo vyenye mamlaka na lugha, vyombo vya habari, taasisi za elimu na vyama vya kitaaluma vya Kiswahili kuendelea kuelimisha watumiaji wa simu na wazungumzaji wa Kiswahili kuthamini lugha yao ya Kiswahili.

### 4.2.4 Kiingereza ni Lugha ya Kimataifa

Watoataarifa wawili kati ya sitini na wanane sawa na asilimia 2.94 walisema kuwa wanatumia Kiingereza kwenye simu kwa sababu ni lugha ya kimataifa. Watoataarifa walisema wanaona Kiingereza kama lugha inayotoka katika nchi zilizoendelea, zinazoheshimika na hutumiwa na watu wengi duniani. Waliongeza kuwa wanakipenda Kiingereza kwa kuwa ni lugha ya kibiashara. Akijaribu kupangilia hadhi za lugha ya Kiingereza na Kiswahili, mtoataarifa mmoja alieleza:

> …Lugha ya Kiswahili ni lugha ya Watanzania tu na sio lugha ya kimataifa, ambapo Kiingereza ni lugha ya kimataifa ni rahisi kurekebisha na kuiendeleza wakati lugha ya Kiswahili inatohoa kutoka Kiingereza. Pia ni rahisi kufanya pragramu za simu yangu katika lugha ya kimataifa na sio lugha ya kitaifa...

Mtoataarifa huyu anaona kwamba lugha ya Kiswahili ina hadhi ya chini kuliko Kiingereza. Yeye anaona fahari kutumia Kiingereza katika simu kwa kuwa ni lugha ya kimataifa. Mtoataarifa huyu anaona kuwa Kiswahili ni kama lugha inayotumika katika eneo dogo, yaani nchini Tanzania kuliko Kiingereza kinachoonekana kutumiwa duniani kote.

Matokeo haya ya watoataarifa yana maana katika hatua ya ustawi na maendeleo ya jamii ya wazungumzaji wa Kiswahili kwa ujumla. Hii ni kwa sababu lugha ndiyo huhifadhi na kurithisha maarifa na uwezo wa kufikiri wa wazungumzaji vizazi kwa vizazi. Kuhusiana na watu kupenda na kuthamini lugha za kigeni, Senkoro (2007) anaeleza kwamba hakuna nchi hata moja duniani iliyopata kuendelea kwa kutumia lugha ya kigeni. Anaongeza kwamba nchi zote tuonazo zikiinukia kimaendeleo leo hii, zimeendelea na zinazidi kuendelea kwa kutumia lugha zao kwa vile masuala yote muhimu yamo katika mawazo yanayoelezwa kikamilifu kwa lugha zao. Tunaungana na mawazo ya Senkoro kwa sababu mbili. Mosi, istilahi za Kiswahili za simu zimefumbata maana zitumiwazo na wazungumzaji wa Kiswahili. Pili, ni jambo linalotia shaka kwa wanazungumzaji wa Kiswahili kujinasibisha na lugha ya Kiingereza kwa kuiona ya thamani na kudunisha matumizi ya Kiswahili

katika simu. Kufanya hivyo ni sawa na kukifukia Kiswahili. Matokeo haya yanatufanya tujenge hoja kwamba ni vigumu kuyafikia maendeleo ya kweli iwapo wazungumzaji wa Kiswahili watakuwa na mwelekeo wa kuthamini na kutumia lugha nyingine isiyo na chembe ya utamaduni wao.

## 5.0 Hitimisho

Makala hii imeonesha kuwa hali ya matumizi ya istilahi za Kiswahili za simu kwa wazungumzaji wa Kiswahili yana masuala mchanganyiko. Imebainika kuwa kuna kiwango cha chini cha matumizi na kukubalika kwa istilahi za simu miongoni mwa wazungumzaji. Aidha, imebainika kuwa wazungumzaji wana sababu mbalimbali za kutumia au kutotumia istilahi za simu. Vilevile, imebainika kuwa baadhi ya masuala ya kinadharia, sifa na misingi ya uundaji wa istilahi hayakutiliwa maanani na waundaji wa istilahi za simu. Makala hii inachokoza na kuchagiza vyombo vilivyopewa dhamana ya kusimamia Kiswahili nchini Tanzania, mathalani, Baraza la Kiswahili la Taifa na Baraza la Kiswahili la Zanzibar, wataalamu na waundaji wa istilahi, kuzipitia istilahi za Kiswahili za simu za mkononi zilizopo ili kuzifanyia marekebisho. Hii ni kwa sababu istilahi hizo zipo tayari kwenye simu na zinatumiwa na baadhi ya wazungumzaji wa Kiswahili wanaotumia simu. Suala la upitiaji upya istilahi za simu litakuwa na tija zaidi kwa kuwashirikisha wazungumzaji wa Kiswahili wanaotumia simu za mkononi. Ushirikishwaji huo unaweza kuwa wa kwenye majopo na kukusanya maoni ili kuwezesha uboreshaji wake. Inatarajiwa kwamba matumizi ya istilahi za Kiswahili za simu za mkononi yataongezeka ikiwa hatua madhubuti zitachukuliwa na wadau wote wa Kiswahili kwa kuwa lugha ya Kiswahili inazidi kukua na kupata msukumo mpya duniani.

## Marejeleo


Crystal, D. (2012). *Spell it Out. The Singular Story of English Spelling*. London: Profile Books.

Felber, H. (1980). “International Standardization of Terminology: Theoretical and Methodological Aspects.” *International Journal of the Sciology of Language*. 23:65-79. Inapatikana katika https://doi/10.1515/ijsl.1980.23. 65/pdf. Ilisomwa tarehe 28/9/2021.

Ibrahim, U.A. (2017). Kiwango cha Ukubalifu wa Istilahi za Kiswahili za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Zanzibar: Mfano Kutoka Istilahi za Kilinux**.** Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Kahigi, K.K. (2007). “Ujanibishaji wa office 2003 na Windows XP kwa Kiswahili Sanifu.” *Kioo Cha Lugha*. 5:70-91.

Kamau S.N. (2007). “A Digital Africa Kiswahili Holds the Key.” *Journal of Language Technology and Entrepreneurship in Africa*. 1:133-143. Inapatikana katika https//www.ajol.if/index.php/article/view/41764. Ilisomwa tarehe 18 Mei 2022.

Kevogo, S.A. (2016). ‘‘Ukuzaji wa Istilahi za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano: Mifano wa Jitihada zisizo Rasmi za Kampuni na Watumiaji wa Simu za Mkononi Nchini Tanzania”. Katika C.L.M. Mwita (Mh.), *Kiswahili na Utandawazi*. Nairobi: Twaweza Communications Ltd. Kur. 151-168.

Kihore, Y.M. (2000). “Makala za Kuchochea Utafiti katika Kiswahili na Teknolojia ya Habari.” *Mulika*. 26:98-105.

Kinyanjui, J.M. (2014). “Challenge of Competing Neologisms: A Case of Kiswahili Technical Terminology”. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Maganga, C. (2008). “Juhudi za Ukuzaji wa Kiswahili Tanzania Bara.” Katika J.G. Kiango G.J. (Mh.) *Ukuzaji wa Istilahi za Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI. Kur. 29-42.

Malangwa, P.S. (2010). “Handling Technical Translations: The Case of Translations of Computer Programs from English into Kiswahili.” Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Malangwa, P.S. (2019). “Neologisms Translated from English into Kiswahili and the Effects Created by the Attitude of the Speakers.” *Kiswahili*. 82: 44-57.

Massamba, D.P.B. (1997). “Problems of Terminology Development: The Case Study of Tanzania.” *Kiswahili*. 59: 86-98.

Massamba, D.P.B. (2008). “Zoezi la Uundaji wa Istilahi katika Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.” Katika J.G. Kiango (Mh.) *Ukuzaji wa Istilahi za Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI. Kur. 100-108.

Mdee, J.S. (1999).‘‘Matumizi ya Istilahi katika Kiswahili na Jinsi Yanavyoathiri Mawasiliano.’’ *Mulika*. 25:37-48.

Nida, E.A. na Taber, C.R. (1969). *The Theory and Practice of Translation*. Leiden: E.J. Brill.

Okyere S.M., Oduori, W.R. na Magugu, V.N. (2016). “Ubinafsishaji wa Dhana Kupitia Tafsiri: Uchanganuzi wa Lugha katika Rununu ya Nokia.” Katika Jilala, H. (Mh.) *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi.* Dares salaam: Daud Publishing Company Limited.

Qorro, M. (2007). ‘‘Matatizo ya Kufundisha kwa Lugha za Kigeni katika Nchi za Afrika: Kwa mfano Kiingereza katika Shule za Sekondari Tanzania’’ Katika Senkoro, F.E.M.K. (Mh.) *Lugha na Fasihi ya Kiswahli Afrika Mashariki*. Dar es Salaam. Chama cha Kiswahili Afrika Mashariki. Kur 54-64.

Sanday, W.A. (2014). “Evaluating the Acceptance and Usability of Kiswahili Localized Mobile Phone App in Kenya: A Case of M-Pesa App”. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Senkoro. F.E.M.K. (2007). “Mauaji ya Halaiki ya Watoto wa Tanzania Kupitia katika Lugha ya Kufundishia Sekondari na Vyuoni.” Katika Senkoro, F.E.M.K (Mh.) *Lugha na Fasihi ya Kiswahili Afrika Mashariki:* Dar es Salaam. Chama cha Kiswahili Afrika Mashariki. Kur. 39-44.

Tumbo-Masabo, Z.N.Z na Mwansoko, H.J.M. (2008). *Kiongozi Cha Uundaji wa Istilahi za Kiswahili.* Dar es Salaam. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.